LUDEWA YETU




# MAANDALIZI YA MRADI WA BOOST YAANZA KUTEKELEZWA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias akishirikiana na Shirika la KLF leo Desemba 21, 2022 wametoa vifaa mbalimbali kwa wanafunzi wa shule ya msingi Milo na shule ya Sekondari Mavala.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo kwa wanafunzi wa shule ya msingi Milo amesema kuwa; "Shirika la KLF wameona umuhimu wa kuwaletea vifaa hivi kama daftari, viatu na Mikoba kwa lengo mwaka 2023 kila mwanafunzi ahakikishe anahudhuria shule na kuongeza bidii ya Kusoma"

Kwa upande wake Mkurugenzi wa shirika la KLF Ally Seif wakati akikabidhi taulo za kike kwa shule ya sekondari ya Mavala amesema kuwa, Kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya wao kama shirika wametambua umuhimu wa kutoa taulo za kike katika shule hiyo kwani zitawasaidia wanafunzi hao Januari 2023 pindi wanaporejea shuleni.

Sambamba na hayo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Sunday Deogratias wakati akizungumza na walimu na viongozi wa maeneo hayo amewasihi kuendelea kuandikisha wanafunzi wapya wa elimu ya awali na darasa la kwanza wa mwaka ujao wa masomo na kuwasimamia vyema wanafunzi wote waliofaulu kuanza masomo yao ya sekondari mwaka 2023.




Kwa upande wake Afisa elimu awali na msingi Bw. Daniel Makorere John amewashukuru viongozi wa shirika la KLF kwa kuona umuhimu wa kutoa vifaa mbalimbali kwa wanafunzi wa shule ya msingi Milo kwani itasaidia kuwahamasisha wanafunzi kusoma na kuhudhuria vipindi kila siku. Amesema; " Kipekee nawashukuruni sana kwa ujio wenu wakati huu wa maandalizi ya sherehe za Krismasi na Mwaka mpya kwa kutoa zawadi hizi kwa wanafunzi. Kipindi kijacho cha mwaka 2023 tumejipanga vyema kuwapokea wanafunzi wapya na mazingira salama ya kuwafundishia wanafunzi hawa yapo tayari, hivyo kila mwanafunzi atasoma katika mazingira salama na tumeanza vyema kutekeleza mradi wa BOOST kwakuanza uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza kwa mwaka mpya 2023 uandikishaji wa wanafunzi wa awali kwa mwaka ujao tulikadiria kuandikisha wanafunzi wa awali 4419 na hadi tarehe ya leo tumeandikisha wanafunzi 4281 ambapo ni sawa na asilimia 96.87, kwa upande wa uandikishaji kwa wanafunzi wa darasa la kwanza tulikadiria kuandikisha wanafunzi 4053 na tumeandikisha wanafunzi 4036 ambapo ni sawa na asilimia 99.43. hivyo kufikia tarehe 31 Desemba 2022 tutakuwa tumeandikisha wanafunzi wa awali na msingi kwa asilimia mia moja. Alisema Mwalimu Daniel Makorere John.


we World


KLF
Kiranja Leadership




MILO

Sambamba na hayo afisa elimu awali na msingi alimaliza kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia fedha halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa ajili ya ujenzi na Uboreshaji wa Madarasa ya shule za msingi na nyumba

## RADI YALETA MAAFA LUDEWA




Wakati Mvua zikiendelea kunyesha kwakuambatana na Upepo mkali na radi Desemba 17, 2022 wilayani Ludewa Mkoani Njombe Mvua iliyoambatana na upepo imesababisha maafa makubwa kwa kuezua nyumba 16 na kusababisha kifo cha mtu mmoja pamoja na mifugo. Maafa hayo yametokea kata ya Luilo katika kijiji cha Lifua.

Viongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Ludewa akiwemo Katibu Tawala wa wilaya ya Ludewa, Mbunge wa Jimbo la Ludewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwapamoja walifika katika eneo la tukio na kushuhudia wahanga wa tukio hilo nalo kisha wakatoa pole kwa wahanga hao.



# WAWEKEZAJI WAENDELEA KUONGEZEKA LUDEWA



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias Desemba 21, 2022 alipokea wawekezaji kutoka Jijini Dar es Salaam waliokuja kwa ajili ya kujitambulisha na kubainisha uwekezaji wanaohitaji kuwekeza ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Kampuni ya A1000 ZERA INVESTMENT yenye makao makuu yake Jijini Dar es Salaam inayojishughulisha na shughuli mbalimbali hapa nchini Tanzania ikiwa ni pamoja na Kilimo imeomba shamba lenye ukubwa wa ekali 750 ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Ludewa ili kufanya uwekezaji wa uzalishaji wa Mbegu za mazao ya Mahindi na Maharage pamoja na uzalishaji wa mahindi lishe kwa ajili ya chakula.







WAWEKEZAJI WA KAMPUNI YA ZERA WAKIANGALIA SHAMBA KWAAJILI YA UWEKEZAJI LIFUA






Shamba kubwa kwaajili ya Kilimo cha Umwagiliaji lililopo Tarafa ya Masasi Kata Luilo linafaa kwa Kilimo cha mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kilimo cha Mpunga, Mahindi, Maharage nk.

Mkurugenzi wa Kampuni hiyo Bw. Joseph John Mwema alisema, Ujio wake ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ni kufanya uwekezaji katika mazao tofauti ila kwa sasa atajikita katika Kilimo cha mahindi na maharage kwenye eneo la bonde la umwagiliaji katika kijiji cha Lifua ambapo anatarajia mara baada taratibu zote za kisheria kukamilika kuanza uwekezaji huo mapema Januari, 2023.

*Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sanday aliwapokea na kusema kuwa, ''Serikali ipo tayari kutoa ushirikiano kwa wawekezaji wote wanaokuja kuwekeza ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, natumia nafasi hii kuwakaribisha Ludewa Wilaya yenye utajiri mkubwa wa maeneo ya uwekezaji wa shughuli za Kilimo. Pia nawaombe mara baada ya kusaini mkataba wa wa uwekezaji wenu muwatumie wananchi wa Wilaya ya Ludewa kwa kuwapa fursa ya ajira kwani hao ndio walinzi wa maeneo hayo na iwe sehemu ya darasa kwa wakulima wanaozunguka maeneo ya mradi huo ili wawe wanufaika na uwekezaji wenu Karibuni sana".*



# LUDEWA TUPO TAYARI KUSHIRIKI TAMASHA LA 9 LA BIASHARA ZANZIBAR.

Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ipo tayari kushiriki Tamasha la 9 la Biashara Zanzibar linalo tarajiwa kuanza rasmi Desemba 30 mwaka huu katika Viwanja vya Maisala Mjini Magharibi.

Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imejipanga vyema kwenda kuwaonesha watanzania na wasio watanzania fursa za uwekezaji zinazo patikana wilayani Ludewa.

“Ludewa ni miongoni mwa wilaya zinazo shiriki Tamasha la 9 la Biashara hapa nchini Tanzania, sisi kama halmashauri tupo tayari na tumefanya maandalizi ya kutosha ili kufanikisha kusudio letu la kutangaza fursa zilizopo Ludewa, naomba niwahakikishie wazanzibar na watanzinia wote kuwa Ludewa tunawaletea fursa na baadhi ya Rasilimali kutoka mpakani mwa Tanzania na Malawi mjipange na karibuni kutembele banda la maonesho la Wilaya ya Ludewa.Alisema Afisa Habari alipokuwa akiongea na vyombo vya Habari.